

TANGAZO LA SERIKALI Na.1022 la tarehe 6/12/2024

SHERIA YA MAMLAKA YA UDHIBITI USAFIRI ARDHINI,
(SURA YA 413)

KANUNI

(Zimetengenezwa chini ya kifungu cha 41(1) (c))

KANUNI ZA MAREKEBISHO YA KANUNI ZA VIGezo NA MASHARTI YA KUTOA HUDUMA ZINAZODHIBITIWA ZA MAMLAKA YA UDHIBITI USAFIRI ARDHINI ZA MWAKA 2024

- Jina
T.S Na.
27 la 2024
- Marekebisho ya kanuni ya 1
- Marekebisho ya kanuni ya 11
TS. Na.
76 la 2020
77 la 2020
- Marekebisho ya kanuni ya 12
1. Kanuni hizi zitajulikana kama Kanuni za Marekebisho ya Kanuni za Vigezo na Masharti ya Kutoa Huduma Zinazodhibitiwa za Mamlaka ya Udhubiti Usafiri Ardhini za mwaka 2024 na zitasomwa pamoja na Kanuni za Vigezo na Masharti ya Kutoa Huduma Zinazodhibitiwa za Mamlaka ya Udhubiti Usafiri Ardhini za mwaka 2024, ambazo katika Kanuni hizi zinarejewa kama “Kanuni kuu”.
 2. Kanuni Kuu zinarekebishwa katika kanuni ya 1 kwa kuingiza maneno “za Usafiri wa Barabara” kati ya maneno “Huduma” na “Zinazodhibitiwa”.
 3. Kanuni Kuu zinarekebishwa katika kanuni ya 11 kwa kuingiza maneno “wa umma au huduma za kubeba mizigo kama zinavyotambulika chini ya Kanuni za Usafiri wa Umma za mwaka 2020 na Kanuni za Usafishaji Mizigo za mwaka 2020” kati ya maneno “usafiri” na “visivyozidi” yaliyopo kwenye kanuni ndogo ya (1) na (2).
 4. Kanuni Kuu zinarekebishwa katika kanuni ya 12, kwa-
 - (a) kubadili maudhui ya kanuni ya 12 kuwa maudhui ya kanuni ndogo ya (1); na
 - (b) kuongeza mara baada ya kanuni ndogo ya (1) kama ilivyobadilishwa, kanuni ndogo ifuatayo:
“(2) Bila kujali kanuni ndogo ya (1), mtoa huduma anayemiliki vyombo vya usafiri wa umma vinavyopungua

vinne anaweza kutoa huduma ya usafiri wa umma iwapo
ataithibitishia Mamlaka uwepo wa makubaliano baina yake
na mtoa huduma mwingine kuhusu utoaji wa huduma ya
usafiri mbadala endapo kutatokea hitilafu ya chombo cha
usafiri au dharura.”.

Dodoma,
11 Novemba, 2024

AHMED MOHAMED AME,
Mwenyekiti wa Bodi